

HATUA ZA UOMBAJI E-PASSPORT

▪ *Kabla ya kujaza Fomu Mwombaji ahakikishe amefanya scanning ya picha yake (passport size) na viambatisho vyote (Cheti cha kuzaliwa, nakala ya passport, cheti cha kuzaliwa cha Baba au Mama na kitambulisho). Viambatisho hivyo viwe kwenye mfumo wa picha (image- jpeg,jng) na kila kiambatishi kisizidi ukubwa wa 1MB. Viambatisho hivyo atatakiwa kuviupload wakati anajaza fomu*

▪ *Awe na kadi yake ya bank ambayo atatumia kufanya malipo wakati wa kujaza fomu hiyo*

▪ *Kwa Waombaji walio miji ya mbali lazima watume bahasha ama Walipie Ubalozini gharama za kutumiwa passport zao zikifika*

1. Mwombaji ajaze fomu online kupitia www.immigration.go.tz (e-services) ataona sehemu ya passport application form

2. Aprint fomu yake na kuituma kwa mail, email (ubalozitanzaniaembassy-us.org) ama kwa kuiwasilisha Ubalozini

3. Ikishapokelewa na kuthibitishwa kwenye mfumo atatumiwa bill ya malipo katika email address aliyojaza kwenye fomu

4. Bill hiyo ya malipo itamwonyesha link ya kufanya malipo kwa njia ya mtandao <https://epay.gepg.go.tz>
5. Kwenye link hiyo ataweka control number na kiasi cha malipo kama Bill inavyoonyesha
6. Akikamilisha malipo atume risiti yake Ubalozini ili malipo yahakikiwe na kupangiwa miadi ya kuja kwa ajili picha na kuchukuliwa alama za vidole
7. Wakati anakuja Ubalozini ahakikishe anakuja na nakala halisi za viambatisho vyake na atapatiwa risiti yake ya malipo
8. Passport ikipokelewa kutoka Uhamiaji Mhusika atatumiwa kwa njia ya mail ama kwa kuchukua mwenyewe Ubalozini.

UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

APRIL 2019

HATUA ZA UOMBAJI ETD

1. Mwombaji ajaze fomu online kupitia www.immigration.go.tz (e-services)
2. Aprint fomu yake na kuituma kwa mail ama kwa kuiwasilisha Ubalozini
3. Ikishapokelewa na kuingizwa na kuthibitishwa atatumiwa bill ya malipo kwa email
4. Risiti ya malipo itamwonyesha link ya kufanya malipo kwa njia ya mtandao
5. Malipo yake yakikamilika na kupokelewa ETD itatolewa
6. ETD husika atatumiwa kwa njia ya mail ama kwa kuchukua mwenyewe.

NOTE:

- *Kwa Waombaji walio miji ya mbali lazima watume bahasha ya kurudishia ETD yake*
- *Kabla ya kujaza Fomu Mwombaji ahakikishe amefanya scanning ya picha yake(blue background) na viambatisho vyote (Cheti cha kuzaliwa, nakala ya passport, cheti cha kuzaliwa cha baba na barua ya maombi).*